

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**KIKAO CHA KUMI NA NANE**

**01 JUNI, 2015**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA ISHIRINI

**KIKAO CHA KUMI NA NANE – TAREHE 01 JUNI, 2015**

### **I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

#### **WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

#### **WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

#### **MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha, 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

## **MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

### **II. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

#### **119. MHESHIMIWA ANNAMERYSTELLA JOHN MALLAC (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-  
Serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi kila mwaka kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Halmashauri za Miji na Wilaya ikiwemo za Mpanda na Sumbawanga ambazo huharibika mara kwa mara kwa sababu ya ukosefu wa mitaro:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutengenezea mitaro hiyo ili kuokoa fedha zinazotumika mara kwa mara kutengeneza barabara zinaposombwa na maji.

**120. MHESHIMIWA DEO HAULE FILIKUNJOMBE (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Maji Safi na Salama ni muhimu kwa afya za Wananchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Maji Safi na Salama katika Mji wa Ludewa.

**121. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Katika Wilaya ya Kasulu ipo miradi ya Maji ambayo ilianzishwa lakini mpaka sasa haijakamilika:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili miradi hiyo iweze kukamilika.

**WIZARA YA MAJI:**

**122. MHESHIMIWA DKT. HAJI HUSSEIN MPONDA (ULANGA MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Mradi wa Maji unaofadhiliwa na Benki ya Dunia; (*phase II World Bank Project*); umepanga kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utaalamu elekezi katika vijiji vya Ngoheranga na Tanga; lakini katika programu zote za Wizara, Vijiji vya Sofi

Mission, Sofi Majiji na Kiswago havikuhusishwa. Katika kukabiliana na changamoto ya tatizo la Maji katika vijiji hivi Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga iliomba kufanyika utafiti, uchimbaji na uwekaji wa pampu katika vijiji hivyo vya Sofi Mission, Sofi Majiji na Kiswago:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa visima hivyo na miundombinu ya usambazaji maji katika vijiji vya Ngoheranga na Tanga;

(b) Je, Serikali ina programu gani ya utekelezaji wa kuwapelekea maji wakazi wa vijiji vilivyosahaulika vya Sofi Mission, Sofi Majiji na Kiswago.

#### **WIZARA YA UCHUKUZI:**

#### **123. MHESHIMIWA SALVATORY NALUYAGA MACHEMULI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:- Meli ya MV Butiama imesimama kufanya kazi kwa muda mrefu sasa:-

(a) Je, ni tatizo gani lililofanya kusimama kufanya kazi kwa meli hiyo;

(b) Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuikarabati meli hiyo.

## **WIZARA YA FEDHA:**

### **124. MHESHIMIWA MUSTAPHA BOAY AKUNAAY (MBULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Kwa nini magari au matrekta ambayo yalikuwa mabovu yanadaiwa leseni ya umiliki wa magari (*motor vehicle licence*) kwa kipindi ambacho magari au matrekta hayo hayakutumika.

### **125. MHESHIMIWA DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALLA (NZEGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuongeza Bajeti ya Afya ili ifikie Azimio la Abuja la asilimia 15.

## **III. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**DODOMA  
01 JUNI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**